RESTLESS DEVELOPMENT

International Budget Partnership

# POLICY BRIEF

## USHIRIKI NA USHIRIKISHWAJI WA VIJANA KATIKA MASUALA YA KODI

Mradi wa Kijana Wajibika – Ijue Kodi Yako, Lipa na Shiriki, unafadhiliwa na International Budget Partnership (IBP), ukiwa na lengo la kuongeza uelewa wa elimu ya kodi na kukuza uwezo wa vijana wa Kitanzania kushiriki katika uchechemuzi na mijadala ya kiraia kuhusu kodi. Lengo kuu la mradi ni kuongeza ushiriki na ushirikishwaji wa vijana ikiwemo vijana wenye ulemavu wakiwa miongoni mwa kundi tengwa ambalo ushiriki wao umekua mdogo katika masuala ya kikodi.

Mradi unalenga kuwajengea uwezo wa kushiriki kikamilifu katika mijadala ya kisera kwamfano; kushiriki katika makongamano ya kodi kitaifa na kikanda, kutoa maoni juu ya mabadiliko ya kodi ili kuongeza ushiriki wao katika majukwaa ya majadiliano, na pia kutoa elimu juu ya nyenzo za uchechemuzi ili kuchangia uwepo wa usawa wa kikodi. Mradi huu unatekelezwa katika Halmashauri tatu za Kibaha Mji, Arusha Jiji na Shinyanga Manispaa kwa kushirikiana na taasisi za vijana ikiwemo; Pwani Youth Network ( PYN), Okoa New Generation (ONG) na Youth and Women Emancipation (YAWE).



Mradi umetoa fursa ya mafunzo kwa vijana 91(54 wakike, 36 wakiume) na 9 (5 wakike, 4 wakiume) kati yao ni vijana wenye ulemavu walio kati ya miaka 15-35 wanaojishughulisha na biashara mbalimbali na kuwajengewa uwezo ambao umeongeza uelewa wao juu ya maswala ya kodi na kuwa mabalozi wazuri kwa vijana wengine kuweza kupata elimu hii na kushiriki kikamilifu.

### MUKTADHA

Usawa wa kikodi ni dhana inayohakikisha kuwa mzigo wa kodi unagawanywa kwa haki kulingana na uwezo wa kila mtu kuchangia, huku mapato yanayotokana na kodi yakitumika kuboresha maisha ya wananchi wote.

Vijana, wakiwemo wenye ulemavu, ni kundi muhimu lenye mchango mkubwa katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii, lakini mara nyingi wanakumbana na changamoto mbalimbali kama; ukosefu wa ajira, elimu ndogo kuhusu kodi, na kutoshirikishwa kwenye maamuzi ya sera za kikodi. Ujumuishaji wa sauti za vijana katika mijadala ya sera za kodi sio tu unaleta usawa wa kijamii, bali pia unasaidia kujenga mfumo wa kodi unaoeleweka, unaowajibika, na unaozingatia mahitaji ya makundi yote.

Kwa kushirikisha vijana katika mchakato huu, Serikali inaweza kuunda sera jumuishi zitakazochochea ushiriki wa vijana ikiwemo vijana wenye ulemavu, kuwawezesha kiuchumi, na kuhakikisha hakuna anayeachwa nyuma.

### LENGO LA UKUSANYAJI WA TAARIFA KUPITIA MAJADILIANO

Restless Development kwa kushirikiana na Okoa New Generation, Pwani Youth Network na Youth and Women emancipation tumefanya majadiliano ya vikundi lengwa (FGD) yaliyoshirikisha vijana 51 (31 wanawake, 20 wanaume ) huku vijana wenye ulemavu wakiwa 4 (wakike) kutoka Halmashauri ya Mji Kibaha, Manispaa ya Shinyanga, na Jiji la Arusha.

Vijana walioshiriki katika majadiliano haya ulizingatia uwakilishi wa vijana wanaojishughulisha na biashara mbalimbali, kubwa, kati na ndogo, baadhi wakiwa wale waliopata mafunzo ya elimu ya kodi na vijana wengine. Majadiliano haya yalilenga kupata taarifa kuhusu mambo makuu matatu;

- Uelewa wa vijana kuhusu masuala ya kodi,
- Ushiriki wao katika ulipaji wa kodi, na
- Ushiriki wao katika mijadala inayohusu kodi.

## Mbinu za ukusanyaji taarifa

Taarifa zimekusanywa kwa kutumia njia ya Majadiliano ya Vikundi Lengwa (FGD) ambapo kulikuwa na mwongozo wenye maswali ya mjadala yaliyoandaliwa kwa mpangilio au mtiririko unaoeleweka ili kupata taarifa za kina juu ya mtazamo wa vijana kuhusu kodi, matarajio kutokana na huduma za jamii zinazotokana na ulipaji wa kodi na kutoa mapendekezo ya kuboresha mfumo ya kodi ili uwe sawa na wa haki kwa makundi yote ya walipa kodi hasa vijana. Zoezi la ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa vilizingatia utafiti wa ubora (Qualitative collection and analysis).

## HALI HALISI; USHIRIKI NA USHIRIKISHWAJI WA VIJANA KWENYE MASUALA YA KODI

Ripoti hii fupi inaonesha hali halisi ya ushiriki na ushirikishwaji wa vijana katika utofauti wa makundi yao kama elimu, umri, aina za biashara wanazofanya, uzoefu wao katika biashara pamoja na hali yao ya ulemavu kwa kuangazia maeneo makuu matatu.

- **UELEWA WA VIJANA KUHUSU KODI**

Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya 2022, idadi ya vijana (wenye umri wa miaka 15–35) inachangia takriban 21.3 milioni ya watu Tanzania. Aidha kundi hili la vijana linachangia katika nguvu kazi ya taifa ambayo ni asilimia 56.9. Wingi huu wa vijana unaonyesha haja ya kuwalenga vijana na kuhakikisha wanafikiwa na elimu ya kodi, kwani mchango wao wa kiuchumi ni muhimu kwa maendeleo ya Taifa.

Tafiti zinaonyesha kuwa viwango vya uelewa wa kodi miongoni mwa vijana nchini Tanzania viko chini. Ripoti ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA, 2021) inaeleza kuwa vijana wengi hawana elimu ya kutosha ya masuala ya kodi ikiwepo, kutambua aina za kodi, manufaa ya kodi, sera mbalimbali zinazohusu kodi na pia wajibu walionao katika kulipa kodi hasa unaotokana na ukosefu wa elimu ya kodi. Kunahitajika uwekezaji wa kimkakati kwenye utoaji wa elimu ya kodi mapema, kupitia mitaala ya elimu na programu za nje ya darasa, ili kuwajengea uelewa wa kina kuhusu ulipaji wa kodi na uwajibikaji wa kifedha.


Kupitia majadiliano yaliyofanyika vijana wamehusisha kodi na masuala mbalimbali kama, kodi ipo kwa faida ya serikali, kodi inaambatana na rushwa na ubadhirifu; huku ikionekana kodi ni fedha zinazoweza kutumika bila kuwa na uwajibikaji, wengine wakahusisha kodi na wizi. Baadhi wakasema kwamba wananchi hawapewi elimu ya kujitosheleza kuhusiana na kodi wala taarifa sahihi hivyo kwa kutokuwa na ufahamu wanaibiwa kwa kutozwa zaidi ya kile wanachostahili kutozwa. Vilevile,baadhi ya vijana wakasema kwamba, Mamlaka ya mapato Tanzania (TRA) kupitia shughuli ya ukusanyaji wa kodi ipo kwa ajili ya kutengeneza hofu na uwoga kwa walipa kodi, kodi ni urasimu. Kijana mmoja akasema,

**"Baada ya kuanza biashara yangu nilikwenda TRA ili kupata makadirio ya kodi kwa ajili ya biashara yangu, lakini kule TRA nilipata mwongozo wa kulipa kodi na sio elimu ya kodi. Elimu ya kodi nimeipata nilipohudhuria kwenye Mafunzo ya kodi (yaliofanyika kwa ushirikiano wa NGOs na Restless Development chini ya mradi wa kijana wajibika.) – Kijana wa kiume-Shinyanga MC**

## IDADI YA VIJANA WALIOSHIRIKI KATIKA MAJADILIANO YA MAKUNDI.




## JUMLA YA WASHIRIKI




- **USHIRIKI WA VIJANA KATIKA ULIPAJI WA KODI**

Pamoja na jitihada za kuboresha mifumo ya kikodi, ushiriki wa vijana, wakiwemo vijana wenye ulemavu, katika ulipaji wa kodi bado uko chini kutokana na changamoto kadhaa za kiuchumi na kijamii.

Vijana wengi wanakabiliwa na ukosefu wa ajira rasmi, hali inayowafanya wasiwe sehemu ya mifumo ya kikodi inayoeleweka. Taarifa ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS, 2021) inaonesha kiwango cha ukosefu wa ajira kwa vijana nchini Tanzania ni asilimia 13.7%. Vijana wengi hufanya kazi katika sekta isiyo rasmi, ambayo mara nyingi inakosa usimamizi wa ulipaji kodi.

Aidha, wengi wao hawana uelewa wa kutosha kuhusu mfumo wa kodi, umuhimu wake, na jinsi ya kushiriki kikamilifu. Kwa upande wa vijana wenye ulemavu, changamoto zinazohusiana na fursa finyu za ajira, ukosefu wa mazingira rafiki ya kiuchumi, na kutengwa katika maamuzi ya sera za kikodi zinazidisha hali hiyo.

Hali kadhalika, mfumo wa kodi haujajikita kikamilifu katika kutoa motisha au unafuu unaowezesha makundi haya kushiriki ipasavyo, jambo linalozuia ushirikishwaji wa vijana na kuendeleza mtazamo wa kodi kama mzigo badala ya nyenzo ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

**VIJANA NAO WALIKUA NA HAYA YA KUSEMA;**

**“Mfumo wa ukusanyaji kodi sio mfumo rahisi na rafiki mara nyingi inasumbua.”**

**“Mimi niweshawahi kujaribu kulipa kodi kupitia simu lakini pesa ilikuwa inarudi”**

“Vijana walisema kuwa, hawashirikishwi kikamilifu katika makadilio ya kodi hasa katika kuelewa jinsi makadilio hayo yanavyofanyika ili kuongeza ulipaji wa kodi kwa hiari.

Vilevile walianisha vikwazo vya kiuchumi, kama vile viwango vya juu vya kodi, hivyo uwezo wa kumudu kulipa kodi kwa wafanyabiashara ni mdogo kutokana na mauzo hafifu hasa wafanyabiashara wenye mitaji midogo kupelekea wao kutumia pesa kuongezea mtaji badala ya kulipa kodi.

Vijana wameainisha uwepo wa changamoto ya mifumo kutokuwa jumuishi hasa kwa makundi yaliyopembezoni hivyo kufanya mchakato wa ulipaji kodi kuwa mgumu.

- **Ushiriki wa vijana katika mijadala inayohusu kodi.**

Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana 2007 toleo la 2024 inasisitiza ushiriki wa vijana katika mipango ya maendeleo ya kitaifa. Hata hivyo, ushiriki wa vijana katika mijadala inayohusu kodi Tanzania bado unakumbwa na changamoto mbalimbali.

Vijana wengi hawashiriki kikamilifu katika masuala ya kodi kutokana na upungufu wa elimu juu ya umuhimu wa kulipa kodi na jinsi kodi inavyosaidia maendeleo ya taifa, ukosefu wa taarifa za majukwaa yaliyopo na wanayoweza kushiriki ili kuchangia katika majadiliano ya kisera yanayohusu kodi pamoja na vijana kutokupata nafasi za maamuzi kwenye mabaraza na majukwaa ya mijadala ya kiuchumi ili sauti zao zisikike. Shirika la Kimataifa la International Budget Partnership (IBP, 2022) linapendekeza kuwepo kwa mashauriano yanayolenga vijana katika michakato ya bajeti na kodi ili kuimarisha uwajibikaji wa kifedha, jambo linalofaa kutiliwa mkazo katika muktadha wa Tanzania.

Hata hivyo vijana walisema kwamba, pamoja na jitihada mbalimbali za serikali kwa kushirikiana na TRA, kutoa taarifa kwa njia mbalimbali mfano Whatsapp, matangazo ya umma, mabonanza na midahalo ya kikanda na wilaya pamoja na kutumia wasanii na watu maarufu kama DJ. Fetty, Edo Kumwembe, Peter Msechu n.k kama mabalozi wa kodi, wamekubali kuwa kama vijana hawajawa mstari wa mbele katika kutafuta taarifa za uwepo wa majukwaa hayo na majadiliano yanayoendelea katika maeneo yao, mfano mijadala inayohusu mapato na matumizi. Pia wameeleza vizuizi mbalimbali wanavyokutana navyo na kuchangia wao kutoshiriki kwenye masuala ya kodi ikiwemo; ukosefu wa majukwaa jumuishi ya kushiriki ili kuelezea maoni yao kwa ufanisi ambako wangeweza kuwa na ushawishi zaidi katika maboresho ya sera za kodi zinazogusa maisha yao ya baadae.

## MATOKEO YA MAJADILIANO NA VIJANA

- **Uelewa mdogo wa masuala ya kodi**

Vijana wengi wameonyesha uelewa mdogo wa masuala ya kodi, ikiwa ni pamoja na aina za kodi, sera za kodi, wajibu walionao katika kulipa kodi na umuhimu wa kulipa kodi katika kutoa huduma za umma. Kukosekana kwa elimu ya kodi na uelewa usio sahihi kuhusu kodi ni changamoto kubwa inayochangia wao kutokuwa na motisha ya kulipa kodi kwa hiari. Mfano, ulipaji wa kodi umefananishwa na wizi, ubadhilifu wa fedha, rushwa na usumbufu.

- **Vizuizi vya ulipaji kodi kwa hiari**

Vijana walieleza kuwa kuna changamoto nyingi zinazowafanya wasilipe kodi kwa hiari, ikiwa ni pamoja na taratibu ngumu na mifumo isiyorafiki hasa kwa kijana anayetaka kuanza biashara, mfumo wa makadilio ya kodi haumvutii kijana kuwajibika kulipa kodi kwani makadilio haya huwa makubwa, uwepo wa kodi nyingi bila kuona manufaa ya moja kwa moja, Mifumo ya marejesho kwa wale walio kwenye biashara inachukua muda mrefu hata siku nzima kuisha. Kukosa imani na mamlaka za kodi sababu ya mambo kadhaa, mfano rushwa inayofanya baadhi ya watu kukwepa kodi hasa wafanyabiashare wakubwa hivyo kuonekana kuwa kodi hainausawa katika ukusanyaji wake hivyo inazuia vijana kushiriki kikamilifu katika kulipa kodi.

- **Ushiriki mdogo wa vijana katika mijadala ya sera za kodi**

Ingawa baadhi ya vijana wachache wanashiriki katika mijadala ya kijamii kuhusu kodi ndani ya vyama vya siasa na baadhi ya ngazi za kiserikali kama Halmashauri, kuna ukosefu wa majukwaa rasmi ya kushiriki kikamilifu katika michakato ya sera hasa majukwaa jumuishi yenye uwakilishi sawa. Ushiriki wa vijana katika mijadala ya sera za kodi ni mdogo, ikionyesha kwamba hawatambuliki vya kutosha katika kuchangia mabadiliko ya kisera kama watanzania ambao pia wako katika mfumo wa ulipaji kodi.

- **Mahitaji ya sera rafiki za kodi kwa vijana**

Vijana walipendekeza kwamba mifumo ya kodi inapaswa kuwa rahisi na kuanzishwa majukwaa rafiki kwa vijana ya kupata taarifa na huduma kupitia vikao vya maendeleo ya kata, mikutano ya hadhara na mitandao pia taarifa za kiwilaya na kimikoa zinazoelezea mapato na matumizi ya kodi. Walielekeza pia kuwa na mifumo ya kidijitali itakayowasaidia kufikia huduma na taarifa za kodi, pamoja na viwango vya kodi vinavyolingana na ukubwa wa biashara za vijana.

- **Usawa kati ya ukusanyaji kodi na utoaji wa huduma kwa jamii**

Kupitia majadiliano haya, imeonesha kwamba vijana wanataka kuona kodi anayoitolewa, inaleta manufaa ya moja kwa moja kuputia uboreshaji wa huduma za kijamii katika maeneo yao mfano, barabara nzuri, huduma za maji, gharama nafuu za maisha, hii itawapa kuona uwajibikaji katika kodi wanazolipa na kushawishika zaidi kulipa kodi kwa hiari. Vijana wanataka kuona miradi inayotekelezeka ambayo inatokana na kodi inaleta tija.

- **Upatikanaji na ufuatiliaji wa taarifa za masuala ya kodi**

Kupitia mahojiano na vijana , tumeona kuwa kwa upande wa vijana wameonesha kutokua na utamaduni wa kutafuta taarifa hasa kama taarifa zinazohusu masuala ya kodi. Lakini pia, hata kwa taarifa zinazotolewa hazifiki kwa upana wake. Mfano, TRA wanapofanya matangazo ya umma yanakua tu ni kwa maeneo madogo yenye mkusanyiko wa watu na kuacha wengine ambao wako pembezoni hivyo kushindwa kupata taarifa kwa wakati. Vijana wamesema kwamba hata kwa taarifa zinazotolewa kwa njia ya vyombo vya habari vimekua vikifikia watu wachache na kuacha wale walioko katika maeneo ya vijijini ambako mara nyingi kuna changamoto za kimtandao na ufikiwaji wa taarifa.

# MAPENDEKEZO

Kupitia majadiliano yaliypfanyika, haya ni baadhi ya mapendekezo yaliyochagizwa na vijana yakilenga utendaji wa pamoja kutoka kwa wadau mbalimbali kama. Serikali, Mamlaka ya Mapato (TRA), mashirika yasiyo ya kiserikali na wadau wa maendeleo pamoja na vijana wenyewe.



## • Mapendekezo kwa Serikali

**1) Uwajibikaji na Uadilifu**

- Kuimarisha mifumo ya kupambana na rushwa.
- Kuhakikisha uwazi katika matumizi ya mapato yanayotokana na kodi.

**2) Mawasiliano**

- Kutumia vyombo vya habari vinavyopendwa na vijana kwa matangazo.
- Kutoa taarifa kwa wakati kuhusu sera na taratibu za kodi.

**3) Msaada kwa Biashara**

- Kutoa punguzo la kodi kwa biashara mpya.
- Kuwasiliana kwa uwazi na jamii kuhusu wajibu wa kodi.

**4) Sera na Sheria**

- Kubadili muda wa neema kutoka miezi sita hadi miezi kumi na mbili kwa biashara inayoanza.
- Kuingiza somo la kodi kwenye mitaala ya shule kuanzia shule za msingi.
- Kuandaa mifumo ya kisheria inayohakikisha ushiriki wa vijana katika utungaji wa sera.

## • Mapendekezo kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)

**1) Kampeni za uhamasishaji**

- Kutangaza masuala ya kodi kupitia vyombo vya habari maarufu kama Wasafi Media.
- Kutumia watu maarufu kuandaa maudhui ya kuvutia kuhusu kodi.
- Kwenye mitandao mfano YouTube yawepo matangazo yenye kuvutia (ya lazima kutazama "ads") na kwenye vipindi vya michezo na tamthiliya.

**2) Sera na uendeshaji**

- Kushirikiana na taasisi za kifedha kuunganisha ulipaji wa kodi na upatikanaji wa mikopo.
- Kuanzisha tuzo kwa walipaji kodi waaminifu kwa makundi mbalimbali kama vijana, walemavu, na kulingana na ukubwa wa kibiashara.
- Kupanua wigo wa walipakodi ( hasa kwa biashara zisizorasmi) ili kupunguza mzigo wa kodi kwa mtu mmoja.

**3) Huduma**

- Kuanzisha madawati ya TRA kuanzia ngazi ya kata ili kurahisisha upatikanaji wa huduma.
- Kurahisisha usajili wa biashara na kutoa muda wa neema wa mwaka mmoja kwa biashara mpya badala ya miezi sita.
- Kuboresha mfumo wa kidigitali unaotumika ili kuondoa changamoto za ufanisi wa kimtandao wakati wa ulipaji wa marejesho (returns)

**4) Marekebisho ya Kisheria**

- Kuhakikisha utekelezaji wa haki wa sheria za kodi bila kufunga biashara kiholela.
- Kuanzisha chombo huru cha kudhibiti ukusanyaji wa kodi.

## Mapendekezo kwa Mashirika yasiyo ya Kiserikali na wadau wa Maendeleo

**1) Programu za Elimu**

- Kushirikiana na shule na vyuo kutoa elimu ya kodi kwa vijana walioko katika mfumo wa shule na programu hizi ziwe za lazima.
- Kufanya mafunzo ya kijamii ili kuongeza uelewa wa masuala ya kodi na kuendesha midahalo kuhusu kodi.
- Kutumia watu maarufu na watengeneza maudhui kuhamasisha juu ya elimu ya kodi na kuwekwa mtandaoni.

**2) Mawasiliano**

- Kutumia vyombo vya habari vinavyopendwa na vijana kwa matangazo.
- Kutoa taarifa kwa wakati kuhusu sera na taratibu za kodi.

**3) Kampeni za Kidijitali**

- Kuandaa maudhui ya kuvutia mitandaoni kama Instagram, YouTube, na WhatsApp, Tiktok
- Kutoa semina za mtandaoni na midahalo kwa vijana yatakayolenga kuongeza uelewa juu ya masuala ya kodi.

**4) Marekebisho ya Kisheria**

- Kuhakikisha utekelezaji wa haki wa sheria za kodi bila kufunga biashara kiholela.
- Kuanzisha chombo huru cha kudhibiti ukusanyaji wa kodi.

**5) Ushiriki wa Jamii**

- Kuwahusisha viongozi wa vijana na wawakilishi wa jamii kueneza elimu ya kodi.
- Kuanzisha kwa majukwaa ya vijana yatakayokua yanajadili masuala ya kodi kuanzia ngazi ya chini yaani Mitaa/Vijiji na Kata.

## Mapendekezo kwa Vijana

**1) Ushiriki wa Kijamii**

- Kushiriki kwenye warsha na programu za elimu ya kodi zinazotolewa na TRA pamoja na wadau mbalimbali.
- Kushiriki mijadala na midahalo kuhusu masuala ya kodi katika jamii mfano, mijadala ya mapato na matumizi

**2) Ujasiliamali**

- Kusajili biashara kihalali na kulipa kodi ipasavyo kwa kuzingatia taratibu na sheria zilizowekwa
- Kutafuta mafunzo na ushauri wa usimamizi wa fedha.

**3) Uongozi na Utetezi**

- Kuchukua nafasi za uongozi kwenye kampeni za elimu ya kodi ili kuwa na uwakilishi wa vijana
- Vijana waliopata elimu kushirikiana na wenzao kuandaa kampeni za kijamii kuhusu kodi.

**4) Huduma za kidijitali:**

- Kufuatilia akaunti rasmi za mitandao ya kijamii kwa taarifa sahihi. Kila kijana kuwajibika kutafuta taarifa zinazohusu masuala ya kodi mtandaoni.

## Hitimisho

**Kuwezesha vijana kushiriki kikamilifu katika mfumo wa kodi ni muhimu katika kukuza utamaduni wa ulipaji kodi kwa hiari na maendeleo endelevu nchini Tanzania. Kwa kurahisisha mifumo ya kodi, kuongeza uelewa, na kuanzisha majukwaa ya ushiriki, vijana wataweza kuchangia kwa ufanisi katika mifumo ya kodi. Ni muhimu kwa wataalamu wa sera kutambua umuhimu wa kushughulikia changamoto za vijana na kutekeleza sera rafiki za kodi zinazochochea ukuaji na maendeleo kwa kila Mtanzania.**

**Ripoti ya Ushirikiano wa Bajeti ya Kimataifa (IBP) ya 2022 inasisitiza umuhimu wa kushirikisha vijana katika michakato ya sera za kifedha ili kuhakikisha utengenezaji wa sera shirikishi na zenye mwitikio. Ushauri wa vijana nchini Tanzania ulilenga kuwashirikisha vijana tangu hatua za mwanzo za miradi ya kodi na kuwapa nafasi ya kutoa maoni kupitia mabaraza ya ushauri, jambo linaloendana na mapendekezo ya IBP. Aidha, ripoti hiyo inaonyesha kuwa kuimarisha uwezo wa vijana kupitia elimu na warsha huchangia uwajibikaji bora wa kifedha. Hii ilithibitishwa na mapendekezo ya vijana ya kuingiza elimu ya kodi katika mitaala ya shule na kutumia mitandao ya kijamii kufikisha elimu hiyo.**

**Vijana pia walipendekeza matumizi ya suluhisho za kidijitali kama vile matangazo kwenye mitandao ya kijamii na miongozo ya kodi inayoweza kupatikana kwa simu, ambayo yanakubaliana na wito wa IBP wa kutumia teknolojia kuongeza uwazi wa bajeti. Ili kuongeza uwajibikaji, vijana walihimiza kuundwa kwa kamati za usimamizi huru wa kodi na hatua madhubuti dhidi ya rushwa. Kwa kuzingatia ulipaji wa kodi, walipendekeza motisha kama ruzuku za biashara na kupunguza viwango vya kodi kwa biashara changa. Ushirikiano huu unaonesha jinsi mapendekezo ya IBP yanaweza kutekelezwa katika muktadha wa Tanzania kwa lengo la kuongeza uwajibikaji wa kifedha miongoni mwa vijana.**


## Ripoti hii imeandaliwa kwa ushirikiano na:

**Na kufadhiliwa na:**



+255 739 773556

Regent Business Park, Wing A, 3rd Floor,
Chwaku/New hub Street, Mikocheni A

https://restlessdevelopment.org/country/tanzania/